

# Unachopaswa kufanya iwapo una matatizo na ARC yako



scottish  
refugee  
council

Aprili 2010

Problems with your ARC - Swahili

Kadi yako ya Ombi la Usajili au 'ARC' ni muhimu. Huonyesha kuwa umetuma ombi la kimbilio na huwa na tondoti zako zote na picha. Inaweza kutumiwa nawe peke yako. ARC yako huthibitisha kitambulisho chako na hukuruhusu kupata msaada wa fedha unaotolewa na Ofisi ya Nyumbani katika Posta iliyoteuliwa.

Kijitabu hiki kinatambulisha la kufanya iwapo ARC yako itaacha kufanya kazi au imepotea au kuibiwa, na jinsi tunavyoweza kukusaidia.

## **Ninapaswa kufanya nini iwapo ARC yangu haifanyi kazi kwenye posta inaojaribu kutoa pesa zangu za usaidizi?**

Iwapo, kwa sababu yoyote, ARC yako haifanyi kaz, pata risiti kutoka kwa mfanyakazi wa posta na ujaribu kutumia kadi tena hiyo wakati mwingine. Ni muhimu kuuliza posta kujaribu kadi yako angalau mara mbili. Unaweza kujaribu baadaye siku hiyo, au siku ifuatayo. *Iwapo kadi yako itakataliwa mara mbili, hakikisha kuwa posta itakupatia risti ya pili.*

Punde unapopata risiti zote, unaweza kuzileta kwa ofisi yetu ambapo tutaweza kukusaidia kuripoti tatizo lako kwa Ofisi ya Nyumbani. Ni muhimu kuwa ulete risiti zote kwa sababu Ofisi ya Nyubani itahitaji thibitisho kuwa umejaribu kupata pesa zako za usaidizi kwa mara mbili bila kufanikiwa. Tafadhali leta risiti hizo mapema kwa wiki kama uwezavyo. *Iwapo utaripoti tu kuhusu tatizo baada ya wiki moja, Ofisi ya Nyumbani haitalipa pesa zozote ulizokosa.*

## **Ninapaswa kufanya nini iwapo ARC yangu imepotea au imeibiwa?**

Iwapo umepotea ARC yako au imeibiwa, lazima kwanza uripoti jambo hili kwa polisi kabla ya kuwasiliana nasi. Utahitaji kupata ripoti ya polisi pamoja na :

- Nambari ya rejeleo la uhalifu huo iliyotolewa na kituo cha polisi (iwapo ulipewa moja);
- Jina na nambari ya ofisa wa polisi aliyerekodi ripoti yako; na
- Jina la kituo cha polisi ulikoripoti.

Wasiliana na Polisi ya Strathclyde katika 0141 532 2000 na watatambulisha polisi yako ya mtaa ambao wataweza kukusaidia kufaili ripoti.

Kisha unaweza kuleta ripoti kwa ofisi yetu na tutakusaidia kujulisha Ofisi ya Nyumbani kuhusu upoteaji huoau wizi. Tafadhali fahamu kuwa ianweza kuchukua wiki kadhaa kutoa ARC mpya. Unapongojea kupata kadi mpya, tunaweza kutuma ombi kuwa Ofisi ya Nyumbani ikutumie Zawadi za Usaidizi za Dharura. Hizi zitatumwa kwa anwani yako ya nyumban kupitia kampuni ya ujumbe inayiotwa DX.

### **Ninapaswa kufanya nini iwapo siwezi kupata usaidizi kwa kutumia ARC yangu kwa sababu niko hospitalini?**

Iwapo umelazwa hospitalini na hutaweza kwenda posta kuchukua pesa zako ukitumia ARC yako, ongea na mfanyakazi wako wa huduma za jamii, kama unaye, au muuguzi kuwasiliana nasi ili tuweze kujulisha Ofisi ya Nyumbani mara moja. Ni muhimu kuwa ufanye hvi haraka iwezekanavyo ili Ofisi ya Nyumbani ijue kuhusu hali yako. Unaweza kupiga **simu yetu ya bure: 0800 085 6087** na uongee na mfanyakazi wa kesi wa zamu. Fahamu kuwa simu yetu ya bure kwa kitumia simu za nyaya pekee.

Iwapo hutatujulisha ili tuweze kuambia Ofisi ya Nyumbani kuhusu mabadiliko katika hali yako, usaidizi wako unaweza kusitishwa, usaidizi wako wa pesa huwezi kupelekwa mbele au kuchukuliwa katika tarehe nyingine. .

### **Ningependa kupata Leseni ya kuendesha ya muda. Ninaweza kutuma ARC yangu kama thibitisho la uraia kwa Wakala wa Leseni za Dereva na Gari (DVLA)?**

**Usitume** ARC yako kwa DVLA kama sehemu ya ombi lako la kupata leseni uendeshaji gari ya kabla. Unahitaji ARC yako ili kuchukua pesa zako za usaidizi kutoka kwa posta kila wiki. Bila hiyo, hutaweza kupokea pesa yoyote.

Kufikia Machi 25, 2010, iwapo utakuwa umetuma ombi la utafutaji kimbilio katika Uingereza na bado hujapokea haki ya kubakia, **hutaweza** kupata leseni ya kuendesha ya Uingereza.

Mabadiliko ya hivi karibuni ya masharti ya serikali yanamaanisha kuwa ni wale waliopewa njia ya haki ya kubakia katika Uingereza **kwa angalau siku 185** watasahili kutoa ombi la leseni ya kuendesha ya Uingereza.

Mabadiliko haya hayaathiri waliotuma ombi la leseni ya uendeshaji ya Uingereza kabla ya Machi 25, 2010.